

# MKATABA WA MAUZO YA KAHAWA GHAFI

Mkataba huu umeingiwa leo tarehe \_\_\_\_\_ Mwezi \_\_\_\_\_ 2020.

## KATI YA

**CHAMA CHA USHIRIKA CHA** ....., S.L.P. ....kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya ..... (ambapo katika mkataba huu kitajulikana kama **"Muuzaji"** maana ambayo itajumuisha warithi na wafilisi wake)

## NA

**Kampuni ya** ....., S.L.P. .... Namba ya usajili ..... (ambayo katika mkataba huu itajulikana kama **"Mnunuzi"** maana ambayo itajumuisha warithi na wafilisi wake)

**KWA KUWA** Muuzaji ni Chama cha Ushirika kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama Vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 na kupewa Namba ya Usajili ..... na kinajihusisha na kilimo cha zao la Kahawa.

**NA KWA KUWA** Mnunuzi ni kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni na ina leseni halali ya kununua kahawa kwa mujibu wa Sheria ya Tasnia ya Kahawa No.23 ya Mwaka 2001.

**KWA KUWA Mnunuzi** anayo nia ya kununua kahawa kutoka kwa **Muuzaji** na kwa kuwa ana miliki kahawa na anayo nia ya kuiuza kwa **Mnunuzi**.

**HIVYO BASI, kwa pamoja pande zote mbili wamekubaliana kama ifuatayo;**

1. Mkataba huu ni wa mauziano ya kahawa ghafi aina ya Kahawa Kavu/Kahawa ya Maganda (Dry Cherry na Parchment coffee).
2. **Muuzaji** amekubali kuuza kahawa yake aina ya ..... kiasi cha kilo ..... Iliyoko kwenye ghala .....
3. **Muuzaji** amekubali kuiuza kahawa yake kwa gharama ya Shilingi za Kitanzania ..... kwa kilo ambayo italipwa na **Mnunuzi**.

4. **Mnunuzi** atawajibika kuisafirisha kahawa kutoka kwenye ghala la **Muuzaji** kwenda kwenye ghala lake au kiwanda cha kukoboa kahawa kwa gharama zake mwenyewe baada ya kukamilisha malipo ya ununuzi wa kahawa hiyo.
5. **Mnunuzi** atawajibika kufanya malipo ya ununuzi wa kahawa hiyo ndani ya siku kumi (10) kuanzia tarehe mkataba huu utakapowasilishwa kwa Mrajisi wa vyama vya Ushirika kwa ajili ya uhakiki.
6. **Mnunuzi** atawajibika kulipa ushuru wa mazao kwa kahawa hiyo kwa Halmashauri ya Wilaya ya ..... kiasi cha asilimia tatu (3%) wakati anafanya malipo ya kahawa hiyo baada ya kupata ankara ya malipo kutoka Halmashauri ya Wilaya ya .....
7. Kwa makubaliano ya mauzo ya kahawa hii, **Mnunuzi** atalipa jumla ya shilingi ..... zitakazolipwa katika Akaunti ya Chama Benki Namba..... iliyopo katika benki ya .....
8. Kwa mauzo ya kahawa hii, **Muuzaji** ambaye ni chama cha ushirika atawajibika kumlipa mkopeshaji wa pembejeo ambaye ni ..... kiasi cha Shilingi za Kitanzania ..... endapo aliwahi kukopeshwa pembejeo.
9. Mkataba huu ni kwa ajili ya ununuzi wa kiasi cha kahawa kilichotajwa kwenye mkataba huu tu.
10. Mkataba huu utakuwa ni wa muda wa miezi/mwaka ..... na utatumika tu kwa msimu wa .....
11. Mkataba huu utanza kutekelezwa mara msimu utakapotangazwa na Bodi ya Kahawa na baada ya kusainiwa na pande zote mbili.
12. Mkataba huu unaweza kukoma muda wowote iwapo Muuzaji au Mnunuzi ataamua kuusitisha baada ya kujiridhisha kwamba Mnunuzi au Muuzaji ameshindwa kutekeleza wajibu wake kwa wakati au amekiuka matakwa ya mkataba huu.
13. Mkataba huu unaweza kupitiwa upya iwapo kutakuwa na ulazima wa kufanya hivyo na iwapo pande zote mbili zitaridhia kwa maandishi na kuridhiwa na Ofisi ya Mrajisi wa Vyama vya Ushirika.
14. Mkataba huu utasimamiwa na kutafsiriwa kwa mujibu wa Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

15. Upande wowote hautawajibika kwa uvunjaji wa mkataba huu ikiwemo kutekeleza wajibu wake chini ya mkataba huu iwapo kutatokea tukio la jambo au janga lisilozuilika (Force Majeure).

16. Iwapo kutatokea mgogoro wowote kuhusiana na Mkataba huu, mgogoro huo utapaswa kusuluhishwa kwa njia ya majadiliano kati ya pande mbili husika; na iwapo majadiliano yatashindikana, utapaswa kusuluhishwa na Bodi ya Kahawa; na iwapo usuluhishi huo utashindwa; mgogoro huo unaweza kutatuliwa kwa pande husika kuchukua hatua stahiki za kisheria.

Makubaliano haya yamefikiwa leo kwa pande zote kutia saini Mkataba huu kwa hiari yao wenyewe baada ya kusoma na kuelewa makubaliano haya kama ifuatavyo:-

**KWA NIABA YA MUZAJI**

Jina: .....  
Wadhifa: .....  
Saini: .....  
Tarehe: .....

Jina: .....  
Wadhifa: .....  
Saini: .....  
Tarehe: .....

**KWA NIABA YA MNUNUZI**

Jina: .....  
Wadhifa: .....  
Saini: .....  
Tarehe: .....

Jina: .....  
Wadhifa: .....  
Saini: .....  
Tarehe: .....

**MKATABA HUU UMESAINIWA MBELE YA:**

**MRAJISI MSAIDIZI WA MKOA:**

Jina: .....  
Mkoa: .....  
Saini: .....  
Tarehe: .....

**BODI YA KAHAWA TANZANIA:**

Mkataba huu umesajiliwa/ haujasajiliwa .....

Jina: .....  
Wadhifa: .....  
Saini: .....  
Tarehe: .....